PAHALI PALIPOANDALIWA KWA AJILI YAKO

UTANGULIZI

Kulikuwa na mtu aitwaye Yesu Kristo ambaye alikuwa ishara ya Mola/Mungu katika mwili wa kibinadamu. Aliiathiri Dunia sana, kiasi kwamba kalenda ya kila mwaka ilibadilishwa na kuwa Kabla ya Kristo na katika mwaka wa Bwana Yesu. Hivyo kalenda ikaanza kuzungukia kwa maisha yake.

Hakufanya tu miujiza wakati alipokuwa akitembea Duniani, bali pia alikubali kusulubiwa kwa ajili yetu. Hivyo ndivyo alipenda sana ulimwengu alioumba. Habari ya kusisimua ni kwamba Bwana Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Neno lake linatwambia kutokana na …..

Matendo ya Mtume 1:3

Wale waliojidhihirisha nafsi yake kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyouhusu Ufalume wa Mungu.

1 Timotheo 3:16

Na bila shaka yo yote, siri ya ndani yetu ni kuu: Alidhihirishwa katika mwili wa binadamu, akajulikana kuwa na haki, akaonekana na malaika, alihubiriwa katika mataifa,akaaminiwa ulimwenguni, akachukuliwa juu katika utukufu.

Yesu kristo alitoa ahadi maalum kwa wote waliomfuata katika maisha haya. Alisema katika…..

Yohana 14:2-3

Nyumbani mwa baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningeliwaambia; maana naenda kuwaandalia pahali. Basi mimi nikienda na kuwandalia, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo

SOMO HILI LINAONYESHA JINSI UNAVYOWEZA KUWA TAYARI……..

MASWALI

Tumia mviringo kuchagua**- Ukweli au Uongo**

Dunia iliadhirika sana na Yesu Kristo kiasi kwamba kalenda ya kila mwaka ilibadilishwa na kuwa kabla ya Yesu Kristo na katika mwaka wa Bwana Yesu.

Ukweli / Uongo

Yesu Kristo alijionyesha akiwa hai baada ya kusulubiwa kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa siku arobaini na kuyanena mambo yaliyohusu ufalume wa mungu.

Ukweli / Uongo

Yesu akawambia wale waliomfuata, " Ninaenda kuwaandalia pahali"

Ukweli / uongo

KUZALIWA TENA

Inaweza kuwa vigumu sana kwa mtu kuelewa kwamba Yesu Kristo amewandalia pahali hao wote ambao wanamfuata . Sababu ya hali hii ni kwamba yeye anazungumzia dhana ya roho. Biblia inasema katika …….

1 Wakorintho 2:14.

Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya roho wa mungu; maana kwake huu ni upuuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.

Kama vile mtoto ambaye hajazaliwa hawezi kufahamu wazazi wake wakimfundisha jinsi ya kukubali upendo wao, huduma zao chakula na makazi, hadi kuzaliwa kwake, vivyo hivyo ni sawa katika roho. Hivyo tufahamu kabisha, kuwa lazima mtu azaliwe tena kiroho.

Ebu, tuone Yesu alimwambia nini mtu mmoja aitwaye Nikodemo ….

Yohana 3:3-7, 9,12.

*Yesu akajibu, akamwambia, amini, amini, nakwambia hakika, mtu asipozaliwa mara ya pili**,** hawezi kuuona ufalume wa mungu. Nikodemo akamwambia eti, inawezekanaje mtu mzima azaliwe? Anawezakuingia tena katika tumbo la mama yake na kuzaliwa mara ya pili? Yesu ajkamjibu, Amini amini nakwambia hakika, mtu asipozaliwa kwa maji na roho, hawezi kuingia ufalume wa Mungu. Mtu huzaliwa kimwili na wazazi wake lakini huzaliwa kiroho na roho wa mungu.*

Kwa hivyo usishangae ninapokwambia kwamba, huna budi kuzaliwamara ya pili. Nikodome akamjibu, akamwambia, yanawezekanaje? Ikiwa hamniamini ninapowambia mambo ya Dunia, mtaniamini nitakapowambia habari za Mbiguni?

HapaYesu anatwambia kwamba ni lazima kuzaliwa tena kwa maji na roho ili tuweze kuingia katika ufalume wa Mungu. Kwa kuwa haiwezekani Mungu kudaganya (Waebrania 6:18), tunaweza kuamini ahadi zake.

Inawezekanaje mtu kuzaliwa mara ya pili? Injili ya Yesu itatuonyesha.

Luka 18:27

Yesu akasema, yasiyowezakana kwa wanadamu, yanawezakana kwa mungu.

Yohana 5:39

Mnayachunguza maandiko kwa bidii kwa maana mnafikiri kuwa humo mtapata uzima wa milele ndani yake. Maandiko hayo hayo ndiyo yanayonishuhudia.

Kwa ufupi tunahitaji kuhakikisha kwamba tunafuata mpango ambao Yesu alitwachia katika uneni wake. Ili tuweze kujiandaa kwa ajili ya pahali alipotuandalia kwa ajili yetu. Anatuwezesha kujua umuhimu wa kutubu na kuamini.

Marko 1:15

Akisema, wakati umefika na ufalume wa mungu kuwa karibu, Tubuni, na kuamini injili.

Mathayo 24:35 *Mbingu na Dunia zitatoweka, lakini maneno yangu hayatapita kamwe* **.**

TOBA NI UAMUZI

“Akili iliyotimamu.”inabidi mtazamo na ufahamu wetu na matendo yetu kuhusu dhambi. Mabadiliko ya kindani katika tabia za mtu yanajionyesha wazi wazi kwa watu wengine na sisi wenyewe tumeamua kumfuata Yesu na kutia maanani maneno yake.

Waromi 6:23

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karamu ya mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Hivyo hatua ya kwanza ya kuokoka ni kutubu na kuamini injili. Hatua inayofuata ni kuzaliwa tena kwa maji na Roho.

MASWALI

Tumia mviringi kuchagua **–Ukweli / Uongo**

Kuona au kuingia katika ufalume wa mungu, mtu lazima azaliwe mara ya pili kwa maji na Roho.

Ukweli / Uongo

Yesu alisema kwamba, muda umefika, na ufalume wa mungu umekaribia: tubu na uamini injili.

Ukweli / Uongo

Kutubu ni hali ya kubadili mtazamo, ufahamu wetu na matendo yetu kuhusu dhambi.

Ukweli / Uongo

Si haja kwetu kuturuhusu maandiko matakatifu eti tuone kama tutakuwa na uzima wa milele.

Ukweli / Uongo

Kwa kuwa mbinguni na Dunia zitatoweka, lakini maneno ya Yesu hayatatoweka, ni muhimu kufuata mpango wake wa wokovu.

Ukweli / Uongo

JINSI YA KUZALIWA KUTOKANA NA MAJI

Mifano ya watu ni chungu nzima katika biblia ambao wamezaliwa mara ya pili kutokana na maji.

Matendo ya mtume 8:30-31

*Ndipo Filipo naye akaanza kusema**,** akitumia maandiko hayo hayo akamhubiria habari njema za Yesu. Walipokuwa wakiendelea na safari wakafika mahali palipokuwa na maji, na Yule towashi akamwambia Filipo, " Tazama hapa **kuna maji** , kuna kitu gani cha kunizuia mimi **nisibatizwe**? Filipo akamwambia, "kama unaamini kwa moyo wako wote unaweza kubatizwa." Akajibu, "Naamini kuwa Yesu Kristo ni mwana wa Mungu." Akaamuru gari lisimamishwe. Wakateremka yule Towashi na Filipo, wakaenda pale kwenye maji. **FIilipo akambatiza**. **Walipotoka kwa yale maji,** Roho wa Bwana akamnyakua Filipo na Yule towashi hakumwona tena. Kwa hivyo akaendelea safari yake akiwa amejawa na furaha.*

Hapa, tunaona mtu akizaliwa kutokana na maji (kubatizwa). Agano Jipya kiasili liliandikwa katika kigiriki kabla ya kutafsiriwa kwa kiingereza. Neno la kigiriki la kubatiza ni "baptizo". Hii ina maana kwamba mwili wote wa mtu unatumbukizwa ndani mwa maji na kuchovya ili kuzidiwa (yaani Mwili mzima uwe kama umenyeshewa na mvua). Yesu alitwambia katika……

Marko 16:16

*Ye yote atakayeamini na kubatizwa ataokolewa. Lakini ye yote atakaye kataa kuamini, atahukumiwa***.**

Hapa kuna mifano mingi ya watu wanaobatizwa (kuzaliwa mara ya pili kutokana na maji) na kile kinachoonyesha wakati walipobatizwa**.**

Matendoya mitume 2:37-41

Sasa, watu waliposikia maneno haya yaliwachoma moyoni, wakawauliza Petro na wale mitume wengine, Tufanye nini ndugu zetu? Petero akawajibu, Tubuni, muache dhambi na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo, ili msamehewe dhambi zenu; nanyi mtapokea zawadi ya roho mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ilitolewa na Mungu kwa ajili yenu na watoto wenu, na wale wote walio mbali, na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu anamwita kwake. Petro aliwasihi kwa maneno mengine mengi na kuwaonya akisema,"jieupusheni na kizazi hiki kiovu." Wote waliopokea ujumbe wa Petro walibatizwa na zaidi ya watu elfu tatu waliongezeka katika kundi la waamini siku hiyo.

Mtume Petro alijua kwamba siyo tu umuhimu wa toba, bali pia kubatizwa kwa jina la Yesu Kristo kwa msamaha wa dhambi. Mifano mingine inapatikana katika;

Matendo ya mitume 8:12

Lakini watu walipomwamini Filipo akihubiri kuhusu Habari Njema za Ufalume wa Mungu, na jina la Yesu Kristo, walibatizwa, waume kwa wake.

Warumi 6:3-4

Au hamfahamu kuwa sisi sote tulibatizwa katika Kristo Yesu, tulibatizwa katika kifo chake? Kwa hivyo tulikufa na kuzikwa naye kwa njia ya ubatizo ili kama kristo alivyofufuka kutoka kwa wafu kwa nguvu na utukufu wa Baba, sisi pia tupate kuishi maisha mapya.

Matendo ya mitume 10:47-48

Je,kuna mtu anayeweza kuzuia watu hawa wasibatizwe? Watu waliopokea roho mtakatifu vile vile kama sisi tulivyoupokea. Kwa hivyo akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo. Wakamsihi Petro akae nao kwa siku kadhaa wa kadhaa.

Kumbuka: Hapa mara nyingine tunaona Maji naUbatizo kwa jina la Bwana (Yesu). Kubatizwa katika jina la Yesu Kristo ni jambo la kusisimua kuzidi jambo jingine lile! Kuwa na msamaha wa dhambi hauwezi kununuliwa kwa kiasi cho chote cha fedha.

Matendo ya mitume 19:5

Waliposikia haya,wakabatizwa katika jina la Bwana Yesu

Matendo ya 2 mitume 22:16

Basi, sasa mbona unakawia? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako kwa kuliitikia jina lake**. (Jina la Bwana ni Yesu)**

MASWALI.

Tumia mviringo kuchagua **–Ukweli / Uongo**

Utapata katika matendo sura ya 8 kwamba Eunch angeweza kufahamu Neno la Mungu bila msaada.

Ukweli / Uongo

Eunch alizama ndani ya maji ili kubatizwa**.**

Ukweli / Uogo

Watu walipouliza nini wanapaswa kufanya,, waliambiwa kutubu na kubatizwa kwa jina la Yesu ili kuondolewa dhambi zao.

Ukweli / Uongo

Walipoamini mahubiri ya Filipo kuhusu ufalme wa mungu na jina la Yesu Kristo, walibatizwa wanaume kwa wanawake.

Ukweli / Uongo

JINSI YA KUZALIWA KUTOKANA NA ROHO

Yesu anatwambia undani wa kinachotokea mtu akizaliwa kutokana na roho. Kwa kweli, huu ni muujiza wa kusisimua, na mamilioni ya watu wanazaliwa kiroho.

Yohane 3:8

Upepo huvuma po pote upendapo. Mvumo wake unausikia lakini huwezi kufahamu unatoka wapi wala unaelekea wapi. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa kwa roho.

Kumbuka: Upepo, roho au pepo katika lugha ya kigiriki ni " phone" sauti, lugha.

Jambo hili linatwambia kwamba mtu ye yote aliyezaliwa na roho (Roho wa Kristo, Roho Mtakatifu, au zimwi tukufu) atasikia sauti (lugha).

Marko 16:17

*Na hizi ndizo ishara zitakazofuatana na hao wanaoamini…. **Watasema kwa lugha mpya.***

Kumbuka: Neno la Yesu linatwambia kwamba ishara inayowafuata wale wanaoamini ni **Kusema kwa lugha mpya.**

Neno la kigiriki "**glossa**" lugha. Thamani ya kuzaliwa kwa roho mtakatifu haiwezi kununuliwa kwa cho chote. Kuna faida nyingi ambazo hupatikana kama matokeo ya kuzaliwa kutokana na Roho.

Isaya 28:11-12

La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa ambao aliwambia, Hii ndiyo raha yetu mpeni mara yeye aliyechoka huku ndiko kuburudika .

Watu wanatufuta kupumzika na kuchangamka na hapa ndipo kwa wale wanaofuata mpango ambao Yesu alitupatia.

Ebu tuangalie faida za kutii Injili.

Yohana 10:10

Mwizi huja kwa nia ya kuiba, kuua, na kuharibu. Nimekuja ili watu wapate uzima; uzima uliokamili.

Mbali na kuwa pahali paliandaliwa kwa wale waliofuata mpango huu, Alikuja ili tuweze kuwa na uzima, na kuwa tuupate kwa chungu tele. Mtu ye yote anaweza kupata wapi faida hizi? Tunahitaji maisha ya milele.

Matendo ya Mitume 1:8

Lakini mtapokea nguvu akishawaachilia Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu-katika Yerusalemu na uyahudi wote na samaria, hadi mwisho wa dunia."

Yesu anatuwezesha kujua kwamba tutapokea nguvu baada ya Roho Mtakatifu kutujia. Kwa kawaida watu wanamsisimko sana baada ya kupokea Roho Mtakatifu kwamba wanataka kuwaambia wengine. Kwa sababu ya nguvu za Roho Mtakatifu, tunaweza kuwa mashahidi.

Matendo ya Mitume 2:1-4

Ilipofika siku ya Pentekoste, waamini wote walikuwa wamekutana mahali pamoja. Ghafla, sauti kama ngurumo kubwa na upepo iliwashukia kutoka mbinguni, ikaijaza nyumba yote walimokuwa wamekaa. Pakatokea kitu kama ndimi za moto ambao uligawanyika ukakaa juu ya kila mmoja wao. Wote walijazwa Roho Mtakatifu wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.

Kumbuka: Neno "ulimi" katika kigiriki ni "glossa" lugha.

Huku ni kuzaliwa kutokana na roho. Walikuwa wote walijazwa na Roho Mtakatifu na wakaanza kuongea kwa lugha mpya, lugha tofauti. Yesu hatuachi tukijibashiria kama tumezaliwa katika Roho (Roho Mtakatifu). Kutakuwa na lugha mpya tutakayopokea na tutajua kwamba sisi ni wazaliwa wa Roho Mtakatifu! ***(Matendo ya Mitume 1:14-15)*** Ebu tuelewe kwamba kulikuwa takribani watu 120 katika siku ya pentekoste kukiwemo Mary mamake Yesu, wanawake na ndugu, wote wakiendelea katika patana moja wakiomba kwa unyenyekevu.

Ebu tuangalie uzoefu wa watu zaidi baada ya kupokea Roho Mtakatifu. Katika miaka iliyofuata mmiminiko wa kwanza.

Matendo ya Mitume 8:14-17

Basi mitume waliokuwa Yerusalemu waliposikia kuwa watu wa Samaria wameamini neno la Bwana, waliwatuma Petro na Yohana waende huko. Nao walipofika waliwaombea ili wapokee Roho Mtakatifu; kwa maana walikuwa wamebatizwa tu katika jina la Bwana Yesu na Roho Mtakatifu ulikuwa bado hajawashukia. Petro na Yohana wakaweka mikono yao juu ya wale waliobatizwa, nao wakapokea Roho Mtakatifu.

Kumbuka: Baada ya Petro na Yohana kupokea Roho Mtakatifu, waliwaombea wengine waweze kupokea kuzaliwa kwa Roho Mtakatifu. Walikuwa tayari wamebatizwa kwa jina la Yesu (aliyezaliwa na maji). Baada ya kuwaombea na kuwaweka mikono kwa vichwa vyao, walipokea Roho mtakatifu. Mfano mwingine unapatikana katika……

Matendo ya Mitume 10: 44-48

Petro alipokuwa akisema maneno hayo, Roho Mtakatifu aliwashukia wote waliokuwa wakisikiliza. Wale waliotahiriwa, walioamini walishangaa, watu wote waliokuja pamoja na petro kwa sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho mtakatifu. Kwa kuwa waliwasikia wakisema kwa lugha mpya na kumtukuza Mungu kwa ukuu wake. Ndipo Petro akajibu, "je, kuna mtu anayeweza kuzuia watu hawa wasibatizwe kwa maji? Wamempokea Roho Mtakatifu kama sisi tulivyompokea." Kwa hivyo akaamuru wabatizwe kwa jina la Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi zaidi kukaa siku kadhaa wa kadhaa.

Hapa kuna mfano mzuri wa kuzaliwa tena. Wakati Petro akiongea, Roho Mtakatifu akaanguka juu ya wote waliosikiliza Neno. Waamini waliokuja pamoja na Petro walishangaa kuona Roho Mtakatifu pia alimwagiwa kwa wanamataifa. (Walijuaje? Mtu hawezi kumwona Roho, lakini walijua kwamba wakati mtu alikutana na Roho Mtakatifu wangeweza kuzungumuza kwa lugha tofauti.) pia walitia maanani amri ya kubatizwa kwa jina la Bwana. (nao wenywe pia walihitaji kuzaliwa kutokana na maji)

Hapa kuna mfano wa mwisho wa watu kadhaa wakizaliwa tena kutokana na maji na Roho, miaka baada ya siku ya Pentekoste. Walipokea roho mtakatifu ushahidi ukiwa uongeaji wa lugha mpya . Kumbuka pia, ingawa walikuwa wamebatizwa, waliposikia ujumbe huo, walibatizwa tena kwa jina la Bwana Yesu.

Matendo ya mitume 19:2-3, 5-7

…….akawauliza, "Mlipoamini mlipokea Roho Mtakatifu?" Wakamjibu, "Hapana. Hatujawai hata kusikia kuwa kuna Roho Mtakatifu." Ndipo Paulo akawauliza, "Mlibatizwa ubatizo gani?" Wakasema, "Ubatizo wa Yohana." Waliposikia haya, wakabatizwa katika jina la Yesu. Na Paulo alipoweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akawashukia, wakasema kwa lugha mpya na kutabiri.

MASWALI

Tumia mviringo kuchagua- **Ukweli au Uongo**

Mtu akizaliwa kutokana na Roho Mtakatifu, kutakuwa na sauti, Neno la kigiriki lililosawa na sauti ni "phone" sauti: lugha.

Ukweli / Uongo

Yesu alitwambia kwamba ishara itakayowafuata wale wanaomini ni kwamba watasema kwa lugha mpya

Ukweli / Uongo

Kuona au kuingia katika ufalme wa Mungu, mtu lazima azaliwe kutokana na Roho Mtakatifu

UKweli / Uongo

Siyo jambo muhimu kama tumezaliwa kutokana na maji na roho tu, muhimu ni sisi pia kuamini

Ukweli / Uongo

Mtu akiwa amezaliwa kutokana na Roho Mtakatifu, ataongea kwa lugha nyingine (lugha tofauti) kipindi Roho akiwezesha kutamka.

Ukweli / Uongo

EBU MJADALA UENDELEA

Pahali pameandaliwa kwa ajili ya wote wanaofuata mpango wa Yesu. Ni nini ambacho mtu anaweza kutoa ili awe na uzima wa milele? ***Marko 8:36***, Yesu aliuliza swali lifuatalo:

Marko 8:36

Mtu atafaidikaje, kama atamiliki ulimwengu mzima, na kupoteza nafsi / maish yake mwenyewe.

Hili ndilo jibu ambalo watu wengi wametamaania! mara tu watu wakionja jinsi kuzaliwa kwa hali chanya na halisi kulivyo, kamwe hawatawai kuwa vile vile, hasa wakiwa kamwe hawaogopi mauti na kwa kweli wataelewa kuwa Yesu amewaandalia pahali wale waliochagua kufuata njia yake.

Matayo 7:24-27

"Basi, kila anayesikiliza haya maneno yangu na kuyatekeleza, atafanana na mtu mwenye busara aliyojenga nyumba yake kwenye mwamba. Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja na upepo ukavuma ukaipiga nyumba hiyo, lakini haikuanguka kwa sababu ilijengwa kwenye msingi imara juu ya mwamba. Na kila anayesika haya maneno yangu na asiyafuate, atafanana na mtu mjinga aliyejenga nyumba yake kwenye mchanga. Mvua ikanyesha, yakatokea mafuriko, na upepo ukavuma ukaipiga hiyo nyumba, nayo ikaanguka kwa kishindo kikubwa."

Faida ambazo Yesu anatoa ni: furaha ambayo haitolewi kifani na iliyojaa utukufu, amani ya Mungu ambayo huzidi ufahamu wa aina yo yote.

Na bora zaidi ya yote, pahali pameandaliwa kwa wale wote ambao watasikiliza Yesu anayoyasema na kuyatimiza.

MASWALI

Tumia mviringo kuchagua- **Ukweli au Uango**

Je, unaona ilivyo umuhimu kuzaliwa kutokana na maji na Roho?

Kweli / Uongo

Kama unaona kuna umuhimu, na ungependa kuwa tayari kwa pahali ambapo pameandaliwa na Yesu basi, ebu tulizungumia suala hili.

Yakobo 4:14

Walakini hamjui litakalotokea kesho! Kwani maisha yenu ni kitu gani? Ninyi ni kama ukungu ambao huonekana kwa muda mfupi tu na baadaye hutoweka.

HAMASISHA INJILI IKAENEZWA

Kwa nakala za ziada na vifaa vyenye uhusiano

www.aplaceprepared.com